MAFAHALI WA KALE WAJITOKEZA

WACHEZAJI wa soka katika enzi za kutoka miaka ya 50 ambao waliwahi kuwakilisha Kombaini ya Mombasa, timu ya Mseto ya Pwani na timu ya taifa ya Kenya katika mashindano kadha wamejitokeza kuanzisha timu yao. Akitangaza habari njema hizo, Bw. Badi Saidi ambaye ndiye mkufunzi wa timu hiyo aliliambia *COASTWEEK* kwamba jina la timu litajulikana kama "Wazee wa Kazi" na ni wale wachezaji waliokuwa maarufu miaka ya nyuma ndio watakaoichezea.

Bw Saidi alizidi kuongeza kuwa wameshaanza mazoezi kabambe ya kujitayarisha kucheza na timu kadha katika Mombasa, katika wilaya nyingine za Pwani na katika sehemu nyingine za Kenya.

Mwalimu huyo wa "Wazee wa Kazi" FC alisema kwamba wameamua kuanzisha timu hiyo ili vijana wanaoinukia wawafahamu wazee wa kale waliokuwa wakilisakata soka la hali ya juu na waliopata kila aina ya sifa.

"Hii itawafanya vijana wa sasa kujiengezea bidii katika mazoezi yao na sina budi kuviambia vilabu vingine vijihadhari kwani tutakuwa tayari kupambana na timu yoyote na musishangae kama mbinu zetu zitawazidia na tutaibuka na ushindi", akaongeza Bw. Saidi.

Alikariri kwamba timu yao ina imani kamili na maongozi yaliyoko kwa wakati huu ya Shirikisho la Soka (K.F.F.) Pwani chini ya uenyekiti wa Bw. Sadla Khamisi. "Tunaihakikishia afisi ya K.F.F. kuwa hatuna nia mbaya nayo kwani tuna uaminifu wa kutosha na tutahitaji msaada ili tujiendeleze", akasema.

Baadhi ya wachezaji ambao wamo katika timu hiyo ni pamoja na aliyekuwa jogoo la Liverpool, Jabir Ali Riziki, Sare, Msuo na miamba kadha ya Feisal akina Ali Kajo, Ahmed Omar na Ahmed Breik. Na wengine wengi ambao wamejitokeza kuihami timu hiyo ya Wazee wa Kazi.

Timu hiyo inafanya mazoezi kila siku ya Jumapili katika uwanja ambapo Feisal inachezea. Mazoezi hayo hufanyika nyakati za asubuhi kuanzia saa mbili hadi saa tano. Wachezaji wa kale wameombwa wajitokeze ili siku chache zijazo waanze kupambana na timu kutoka ngazi za chini hadi baadaye ichuane na timu zilizoko katika supaligi.

AHSANTE RAIS

• *BW. SALIM*

MGOMBEA kiti cha udiwani katika eneo la Kongowea, Bw. Khalef Salim amemshukuru Mtukufu Rais Moi pamoja na chama cha Kanu kwa kumuidhinisha na kumpatia kibali kuwa mmoja wa wapigania wa kiti hicho cha Kongowea mjini Mombasa.

Katika taarifa yake, Bw. Salim alisema: "Nitajitolea nikishirikiana na Kanu katika kuendeleza maendeleo nchini kwa njia ya amani, upendo na umoja ili kutimiza yale Mtukufu Rais Moi anatutaka viongozi tufuate mwito wake wa filosofia Nyayo kwa vitendo".

Mkuu wa Polisi Mkoani Pwani, Bw. Kamau (katikati) anaonekana akiongea na mwenyekiti wa kamati wa ASK Pwani, Bw. G. Kassim Owango (kushoto) hali mwenyekiti mdogo, Bw. Brown Ondego (kulia) na maafisa kadha wakiangalia wakati alipotembelea uwanja wa maonyesho wiki iliyopita.

PICHA: CAESAR MADDANGANHA

HARUSI ya kufana ilifanyika katika ukumbi mpya wa Ujamaa Social Club, Majengo mjini Mombasa. Bw. Harusi, **Abdu Rizik Abeid Farhan** *ambaye ni mwanachama wa Black Panther FC anayefanya kazi Saudi Arabia anatunukiwa zawadi na mwenyekiti wa klabu hiyo,* **Bw. Omar Maulana**.

Asemavyo Mhariri:

K.F.F. TAWI LA PWANI WASIWASAHAU "WAZEE WA KAZI"

KATIKA UKURASA huu tumeichapisha habari fupi kuhusu timu ya kandanda iliyoanzishwa hivi karibuni ikiwa na wachezaji wengi maarufu wa enzi zilizopita; wachezaji ambao wengi kati yao waliwahi kuliwakilisha taifa letu katika mapambano kadha ya kimataifa na waanzilishi wa timu hiyo wameipa jina la **Wazee wa Kazi**.

Hakika kuanzishwa kwa timu hii ni jambo la maana la kuwakumbusha vijana ambao wanainukia kwa wakati huu ni akina nani na ni miamba gani walikuwa maarufu katika enziza miaka kutoka, 50, 60, 70 na mwanzoni mwa miaka hii ya 80. Hakika kwa kuwa kama alivyotufahamisha Ikocha: wa timu hiyo, **Bw. Badi Saidi** kuwa wako nyuma ya Shirikisho la Soka (K.F.F.) Pwani, hakuna la kutia shaka kama kuanzishwa kwa timu hiyo kuna nia mbaya yoyote.

Jambo la kufurahisha zaidi ni maelezo ya Bw. Saidi ambaye alitufahamisha kwamba wanasoka hao wa "kale" wameshaanza mazoezi kabambe na wako tayari kuchuana na vilabu kadha vya hapa Pwani pamoja na vilabu vingine katika kila pembe ya Kenya. Jambo la kufurahisha pia limejitokeza na kama alivyonifahamisha mmoja kati ya wachezaji wa timu hiyo kwamba watakuwa tayari kuvisaidia vilabu vichanga vipate kujiendeleza.

Kuna baadhi ya wachezaji wa sasa hawawafahamu akina **Jabir Ali Riziki**, Ahmed Breik, Raphael Omollo, Said Badi, Khamis Ali, Ali Kajo, Ahmed Omar kama walikuwa baadhi ya wanasoka waliowika nyakati hizo na hata kama wanawajua kwa sura, hawakujua ni sifa gani baadhi yao na wengine ambao sikuwataja walikuwa nazo katika ukumbi wa soka.

Niwajibu wa K.F.F. Pwani kufanya kila liwezekanalo kuona timu hii inadumishwa na wachezaji wake wanapewa heshima ya kuruhusiwa kuona michuano yote yanayofanyika katika stadium ya Mombasa kwani wamepoteza muda mwingi wa maisha yao katika kulisakata soka la hali ya juu; na ni wao ambao walifanya uwezekano hata wakapatia mkoa wa Pwani na Kenya sifa katika mechi kadha.

Kama nia ya timu hiyo ni kusaidia vilabu vinavyoinukia na pia kuisaidia K.F.F. kwa njia ya kujitafutia fedha za kuendeleza soka mkoani, basi nayo K.F.F. inastahili kuisaidia katika kuijenga timu hii ambayo nina uhakika baada ya mwezi mmoja ama miwili, huenda ikawika kuliko baadhi ya timu tulizonanzo wakati huu.

Mashabiki wa soka kote Mkoani Pwani pamoja na mashirika na makampuni ya binafsi wajitolee kuona timu hii inafaulu katika lengo lake. Vifaa vya kuchezea soka kama viatu, jezi na mahitaji muhimu ni baadhi ya misaada ambayo timu hii inastahili kuyapata na nina uhakika wako watakaojitolea kuona "Wazee wa Kazi" wanajiendeleza ili wapate kutuonyesha mbinu za kale la kulisakata kabumbu!

ABDULRAHMAN SHERIFF

★★★★★★★★★★★★★★★★★

HAKUKUWA NA MSAMAHA TENA - SI GHARKA HIYO!

GHARKA - MAFURIKO: AMRI ya Mwenye-ezi-Mungu ikapita, hakukuwa na msamaha tena wala toba! Hakukubaki hata thuluthi ya ardhi ambayo haikufinikwa na maji! Kulinyesha na kunyesha kama kwamba mbingu ni chungio! Hata ardhi haikuweza kuyanzuilia maji hayo, mafuriko yalipanda mpaka yakawazingira watu wale waovu kutoka kila upande!

Mwenye ezi Mungu akamteremshia wahyi Nabii Nuh akamwambia, "Wachukuwe walio amini katika watu wako, pamoja na jamii yako katikas safina hiyo". Na alimwambia achukue mnyama na ndege wawili wawili, mke na mume kwenye safina hiyo. Kwani mafuriko hayo yalizingira kila kitu, hapakuwa na mtu wala mnyama aliyeweza kunusurika.

Nuh (A.S.) akafanya kama alivyoamrishwa, wale walioamini kati yao pamoja na jamii yake na jike na dume la wanyama na ndege. Safina hiyo ikaolea kwenye mawimbi makali. Ikapanda mawimbi kama kwamba ni milima mrefu. Na wale mafasiki wakapanda kwenye vilima na mahali palipo paa kukimbia hayo mafuriko, lakini wapi! Siku hiyo hakukuwa na pakukimbilia wala hawakuweza kukimbilia radda ya Mwenye ezi-Mungu isipokuwa kurudi kwake yeye Mola.

MTOTO WA NUH: MIONGONI mwa wale waliokataa kuamini alikuwamo mtoto wa Nuh wa kiume. Roho ya uzazi ikampiga Nuh, bila shaka namna ya mtu atakavyo mchukia mtoto wake lakini akifikwa na maafa lazima mzazi atataharaki. Basi Nabii Nuh hakuweza kustahamili akamwita. "Ewe mwanangu njoo na sisi katika Safina hii, usende na hao mafasiki!" Mwanae akamjibu, "nitakwenda kwenye mlima mkubwa, na huko mafuriko hayatanifikia".

Nuh zkamjibu, "Leo hakuna mtu atakayenusurika na ghadhabu za Mwenye-ezi-Mungu isipokuwa wale aliowarehemu" na hapo hapo mawimbi yaliwatenganisha Nuh na mwanae na mtoto wake akawa pamoja na wale walioangamia. Nuh akahuzunika sana na akataka mwanae aepushwe na moto na aingie peponi ijapokuwa hakuweza kuokolewa na mafuriko hayo pamoja na adhabu ya kufufuliwa kuwa kubwa zaidi.

Hata hivyo Nuh akakumbuka ahadi ya Mwenye-ezi-Mungu aliyompa ya kuwanusuru jamii yake na Mungu havunji ahadi yake. Kwa hivyo Nabii Nuh akakata shauri kumuombea mwanae kwa Mwenye-ezi-Mungu.

★★★★★★★★

Je, itakuwaje juu ya ombi la Nabii Nuh kwa Mola wake kuhusu msamaha kwa mwanae? Yote utayapata katika sehemu ya mwisho ya makala haya ambayo yametayarishwa na Aisha A. Omar katika sehemu zake mbili za mwisho zenye vichwa: "Mtoto wako sikatika wema" na "Baada ya Mafuriko". Kwa hivyo fahamu Safina ya Nuh itamalizikia wapi katika **COASTWEEK** *wiki ijayo.*

Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI
VYA FARUCCI KWA MSHINDI
WA KWANZA NA T-SHIRT
KWA WASHINDI WA PILI
NA WATATU KATIKA SHINDANO
JIPYA LA KUJAZA MANENO
SWAHILI CROSSWORD No. 169

KWENDA KULIA:

1. Chombo cha kutizamia viini vya ugonjwa
6. Shika, kamata.
7. Toa idhini
8. Kungwaa
9. Jina la kike
10. Aina ya ndege
12. Angalia, fungua macho
15. Funga ndoa
16. Ufupi wa "Lengo Hasa".
17. Ota, chipuza.
18. Bembeleza.

KWENDA CHINI:

1. Sehemu iliyo wazi ya hewa katika nyumba.
2. ....ndio ukufunzao.
3. Simama
4. Amerika ya kaskazini
5. Alama, mpaka
11. Jina la kiarabu
13. Namna ya mdudu hatari
14. Vuno
16. Neno la kumaka.

Washinidi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 168.

1. Ahmed Mosin, Sanduku la Posta 112, MALINDI

2. Miss Jane Pili, Sanduku la Posta 90204, MOMBASA.

3. Idris Ramadhan, Sanduku la Posta, 98841, MOMBASA.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 168.

KWENDA KULIA

1. SEBULE, 4. US, 6. NARANDA, 7. KU, 8. ADUI, 9. AL, 10. RAHISI, 12. UCHI, 14. ANUA, 16. UK, 17. ILIKI, 18. AUA.

KWENDA CHINI

1. SANDARUSI, 2. UJASIRI, 3. ENDESHA, 5. SIMULIA, 7. KASUKU, 11. INUA, 13. HII, 15. NI.



JINA.......................................

SANDUKU LA POSTA..........................

....

Shindano la Fumbo La Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwe Muhariri COASTWEEK Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatono tarehe Septe 14, 1983, saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.